# SHULE YA KITAIFA, MARANDA

**Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)**

## MTIHANI WA MWIGO, 2025

**102/3** **KISWAHILI (Fasihi)** **Karatasi ya 3**

# MWONGOZO

# SIRI

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. Lazima**

***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Ndimi Kisoi, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani
Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ana, gozi kusakata nami

Kijiji kizima kilinijua
Mimi ndiye **Simba wa Yuda**
Ukipenda **Haile Selasia**
Wazee walinienzi
Wakamiminika kiamboni
Mabinti kunikabidhi

a) i) Tambua kipera kilichokolezwa kwenye kifungu hiki. (alama 1)

***Lakabu***

*1x1=1*

ii) Eleza sifa **nne** za kipera ulichokitambua. (alama 4)

i. *Hutumia taswira-simba*
ii. *Huwa majina ya kupangwa- Haile Selasia*
iii. *Ikidumu huweza kuwa kama jina la mtu kisha jina halisi kusahaulika- Sonko.*
iv. *Huambatana na sifa za mhusika – Sonko.*
v. *Huweza kuwa neno au fungu la maneno-Simba wa Yuda*
vi. *Huwa na maana fiche.*

*4x1=4 (bila mifano tuza 0)*

b) Tambua shughuli **mbili** za kijamii zinazojitokeza kwenye kifungu hiki. (alama 2)

i. *Ufugaji – makoo, madume*
ii. *Ndoa/Harusi/Sherehe/Kukongamana* - *Mabinti kunikabidhi*
iii. *Uchezaji ngoma/usogora* - *Wachezaji hodari wa ngoma*

*2x1=2*

c) Fafanua njia **nne** ambazo kwazo fasihi simulizi imeathiri fasihi andishi. (alama 4)

i. ***<u>Maudhui</u>*** *– baadhi ya masuala yanayoshughulikiwa katika fasihi simulizi ndiyo yanayoshughulikiwa katika fasihi andishi. Maudhui yanayoangazia maadili katika jamii kama vile ubinafsi, usaliti, ufisadi na mengine kama uwajibikaji na bidii yananagaziwa kote.*
ii. ***<u>Dhamira</u>*** *– lengo la fasihi simulizi ni sawa na fasihi andishi hivi kwamba zote huadilisha, kuelimisha, kukuza utamaduni ikiwemo malengo mengine. Zinalenga kuwasilisha masuala yanayomzunguka binadamu kupitia sanaa.*
iii. ***<u>Nyenzo na malighafi</u>*** *– zote hutumia lugha kupitisha jumbe. Fasihi simulizi hutumia sana viziadalugha huku simulizi ikitumia tamathali za usemi na mbinu za kimtindo.*

**©Kamati Andalizi ya Mwigo, Maranda, 2025**

iv. ***Usimulizi*** – *msingi wa fasihi simulizi ni masimlizi. Baadhi ya kazi za fasihi andishi zina masimulizi yanayoendeshwa kupitia nafsi ya kwanza au tatu.*
v. ***Utendaji*** – *fasihi simulizi ni tendi. Vivyo hivyo, kuna baadhi ya vipera vya fasihi andishi ambavyo vimechukua utendaji huo kama vile tamthilia.*
**vi. *Fani***
a) ***Ploti*** – *fasihi andishi imechukua fani ya mtiririko wa vitushi kutoka kwa fasihi simulizi. Kazi za fasihi andishi huwa na muwala sawa na za fasihi simulizi.*
b) ***Wahusika*** – *fasihi andishi hivi leo hutumia wahusika walioachiwa fasihi simulizi kama vile wanyama, mazimwi, mizimu na hata mimea. Uvumbuzi wa maandishi umepelekea aina hizi za fasihi kuathiriana kiuhusika.*
c) ***Nyimbo*** – *mtambaji wa ngano kwa kawaida hutumia nyimbo. Vilevile, kazi nyingi za fasihi andishi sasa zimekumbatia nyimbo. Kazi kama vile riwaya nyingi na hadithi fupi zimeshirikisha matumizi ya kipengele hicho.*
d) ***Fantasia*** – *hupatikana katika baadhi ya ngano. Katika ulimwengu wa fasihi andishi, kuna baadhi ya riwaya, tamthilia na hata hadithi fupi zenye mandhari dhdhnia/za kifantasia.*
e) ***Safari*** – *motifu ya safari, ambayo awali ilijitokeza katika kazi za fasihi simulizi pekee kama ngano sasa zinadhihirika katika fasihi andishi.*

*Za kwanza 4x1=4*

d) Eleza **umuhimu** wa hojaji katika kukusanya data za fasihi simulizi. (alama 5)

i. ***Gharama ya chini***-*maswali yanaweza tumwa na kujibiwa bila kusafiri hadi eneo*
ii. *Mtafiti* ***anaweza kufikia idadi kubwa ya watoaji habari kwa kipindi kifupi*** *kwa sababu hojaji nyingi zinaweza kutumwa hata kwa njia ya posta.*
iii. ***Yaweza kutumika katika mahojiano*** *kama mwongozo; kufidia udhaifu wa mhojiwa.*
iv. ***Humpa mhojiwa muda wa kuwazia maswali*** *na kufanya uchunguzi kabla ya kujibu.*
v. *Hojaji kwa kawaida* ***hazina athari za mtafiti*** *kwa vile hayupo zinapojazwa.*
vi. ***Huweza kubadilishwa kulingana na kiwango*** *cha wajazaji au wahojiwa.*
vii. ***Huokoa muda***-*mhoji anaweza kuiacha kwa mhojiwa ijazwe bila kusubiri.*
viii. ***Husaidia kupata majibu ya siri*** *ambayo mhojiwa anaogopa kutoa.*

*Zozote 5x1=5*

e) Bainisha namna mtaala wa elimu unavyokuza fasihi simulizi shuleni. (alama 4)

i. *Mtaala* ***umeshirikisha somo la fasihi simulizi*** *kufundishwa shuleni.*
ii. *Umepelekea* ***kuajiriwa kwa walimu*** *wanaofundisha somo la fasihi simlizi shuleni.*
iii. *Umepelekea* ***kuchapishwa kwa vitabu vya fasihi simulizi*** *vinavyotumika katika viwango mbalimbali vya elimu katika shule mbalimbali nchini.*
iv. *Umetoa nafasi ya kuwepo kwa* ***mashindano yanayoendana na mitaala ya sanaa na muziki*** *kila mwaka katika viwango mbalimbali mpaka vya kitaifa.*
v. *Umepelekea* ***utafiti zaidi*** *kufanywa katika vyuo vikuu na vya kiufundi kuhusu fasihi simulizi.*
vi. *Mtaala umefanya serikali* ***kutenga mgao*** *katika bajeti wa kuangazia masuala ya fasihi simulizi na turathi za jamii.*

vii. ***Kuimba gwarideni/maabadani*** *kama sehemu ya mtaala shuleni.*
viii. ***Sanaa ya ngoma/ngomezi*** *inaambatanishwa na uimbaji wa nyimbo za kitaifa/kizalendo.*
ix. ***Kengele*** *hutumiwa shuleni kuongoza/kuratibisha utekelezaji mitaala shuleni.*

*Zozote 4x1=4*

## SEHEMU B: RIWAYA

**Clara Momanyi**: *Nguu za Jadi*

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.** a) "Ikiwa mmoja wa hawa wenzangu atadhurika, nitamwaga mtama. Liwe liwalo."

i. Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)

*Msemaji ni* ***Ngoswe*** *akimwambia* ***Sagilu*** ***nyumbani kwake*** *Mtemi Lesulia. Hii ni baada ya Ngoswe* ***kutofautiana nao kuhusina na njama potovu****.(uk 129)*

*4x1=4*

ii. Eleza athari **nne** za msemaji kumwaga mtama ukirejelea riwaya ya *Nguu za Jadi*. (alama 4)

i. *Ngoswe anamripoti Sagilu kuwa ana uhusiano na Cheiya hivyo basi* ***kuharibu uhusiano wa Sagilu na Mashauri****.*
ii. *Mangwasha anapopata stakabadhi za ardhi anazirudufisha na* ***kusababisha wao kushinda kesi kortini ya ardhi yao****.*
iii. *Inapojulikana kuwa Mtemi Lesulia alimteka nyara Lonare wafuasi wake* ***wanakosa kumpa kura*** *hivyo basi Lonare anashinda kwenye uchaguzi.*
iv. ***Biashara ya Sihaba kuwatumia wasichana wadogo katika ufuska inatibuka*** *na anaishia kufungwa.*
v. *Chifu Mshabaha anagunduliwa kunyakua shamba la Lonare anapokuwa kiongozi* ***ananyang'anywa ardhi hiyo****.*
vi. *Baada ya Cheiya kutambuliwa na Ngoswe kuwa ana uhusiano na Sagilu* ***inasababisha ndoa yao na Mashauri kuvunjika****.*
vii. *Baada ya kubainika kuwa Ngoswe si mtoto wa Lesulia ila ni wa Sagilu* ***inasababisha uhusiano wao kuvurugika na kuwasambaratisha****.*
**viii.** *Mangwasha anapobaini kuwa Sagilu ndiye anampa Mrima pesa za kuenda Ponda Mali* ***anazirudisha kwake hivyo basi kukatisha kupokea pesa zaidi za starehe kwa Mrima.***

*Zozote 4x1=4*

b) "Hivyo ndivyo ulivyofunzwa na mamako? Ama kweli, wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee." *(uk 40)*

Kwa hoja **kumi na mbili**, thibitisha ukweli wa kauli iliyopigwa mstari ukirejelea riwaya *Nguu za Jadi*. (alama 12)

i. ***Kufuata waume zao wanakobarizi*** **-** *Mangwasha anamfuata Mrima Ponda Mali licha ya mila na tamaduni kumkataza kufanya hivyo.*
ii. ***Kujichagulia mchumba*** *– Licha ya shihinikizo za Chifu Mshabaha kuwa akubali rai za Sagilu, Mangwasha anajichagulia Mrima na hata kuambaa mkahawa wa Mpenda Bure/Mangwasha anakataa kuwa kimada wa Sagilu licha ya mila na tamaduni kumnyima mwanamke uhuru wa kujichagulia mchumba.*

iii. ***Kujiendeleza kimasomo*** *– Mangwasha anaendeleza masomo yake baada ya shule ya upili na kufuzu. Wanawake wengi wanakosa kufanya hivyo kwa sababu ya mila. Inambidi kumshawishi babake Mzee Shauri kumsaidia kuendeleza masomo yake licha ya alama zake kutomruhusu kufanya hivyo. (uk 14)*
iv. ***Kumtunza Mrima anapougua*** *– Mangwasha anamtunza Mrima anapougua baada ya kujiingiza katika pombe haramu kinyume na mila.*
v. ***Kukaidi amri zinazoendeleza ukabila ofisini*** *– Mangwasha anakataa kufuata amri zinazoendelza ukabila ofisini mwa Chifu Mshabaha licha ya tamaduni kumkataza kukaidi amri za bosi wake.*
vi. ***Kushauriana na wanaume jinsi ya kuendesha familia*** *– Mangwasha anashauriana na Mrima kuhusu namna watoto wanavyofaa kulelewa. Mila zinamwachia mwanaume jukumu la kuamua.*
vii. ***Kujitwika malezi*** *– Mangwasha anakimu mahitaji ya Sayore na Kajewa Mrima anapopotelea Ponda Mali licha ya mila na tamaduni kumtwika mwanaume jukumu hilo.*
viii. ***Kumfanyia Lonare kampeni*** *– Mangwasha, Mbungulu na wanawake wengine wanamfanyia Lonare kampeni licha ya mila na tamaduni kusema kuwa mwanamke anapaswa tu kuonekana bali asiskike.*
ix. ***Kuzuia ufisadi*** *– Mangwasha anamshurutisha Mrima kurudisha pesa haramu anazopewa na Sagilu licha ya mila kumzuia mwanamke kumshurutisha mwanaume kufanya kitendo chochote kile.*
x. ***Kufanya kazi/kuajiriwa afisini*** *– Anafanya kazi kwa Chifu Mshabaha licha ya kuwa Mketwa. Tamaduni ziliwabana Waketwa, zikatengea Wakule ajira hizo.*
xi. ***Kuhamasisha na kuhutubia umma*** *– Mangwasha anawahamasisha watu na kuwahutubia nje ya kanisa licha ya mila kumnyima mwanamke fursa hiyo.*
xii. ***Kumsaili mumewe*** *– Mangwasha anamwuuliza Mrima alikotoka na iwapo Sagilu anamtafutia mke mwingine, tukio ambalo ni mwiko kulingana na mila. (uk 41)*
xiii. ***Kufungulia wachumba wao biashara*** *– Mangwasha anamfungulia Mrima biashara. Ni kinyume na mila inayosema kuwa ni mwanaume anayepaswa kukimu mahitaji ya mkewe na wanawe.*
xiv. ***Kuanzisha miradi ya kusaidia vijana*** *– Mangwasha anaanzisha miradi ya kuwasaidia vijana licha ya mila kuwapa wanawake nafasi finyu sana katika maendeleo ya Wahafidhina.*
xv. ***Kufunga danguro la Sihaba*** *– Mangwasha, Mbungulu na wanawake wengine wanaandamana na kufunga danguro la Sihaba ambako aliendeleza ufuska wa vigoli waliofaa kuwa shuleni licha ya mila kumpa mwanamke nafasi finyu.*
xvi. ***Kuongoza maandamano*** *– Mangwasha, Mbungulu na wanawake wengine Waketwa wanawaongoza Waketwa wenzao wakiimba nyimbo za ukombozi wakirejea katika ardhi yao walikokuwa wamefurushwa Matango.*
xvii. ***Cheiya anahusiana kimapenzi na Sagilu*** *– licha ya Sagilu kuwa Baba Mkwe wake/kuwa mchumba wa mwanawe Sagilu (Mashauri).*
xviii. ***Nanzia anamwendea kinyume Mtemi Lesulia*** *- anamwendea kinyume na Sagilu hivyo kupelekea kuzaliwa kwa Ngoswe kinyume na mila.*
xix. ***Ushuhuba pasi kuchumbiana*** *– Sagilu na Sihaba wana mahusiano pasi kufunga ndoa. Sihaba alimpa Sagilu kila atakalo naye Sagilu alimmiminia hela.*

***Za kwanza 12x1=12 (asiporejelea mila/tamaduni/itikadi, atuzwe 0)***

**3.** a) "Hata huyo Lesulia unajuaje atakuwa mtemi wetu tena? Umeishi ndani ya kivuli cha Lesulia kiasi cha kwamba hujui uchaguzi unabisha? Umo ndotoni wewe! Aliye juu msubiri chini, kaka. Wavyele hawakukosea waliposema ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni."

Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 6)

i. ***Balagha***-*Hata huyo Lesulia unajuaje atakuwa mtemi wetu tena?*
ii. ***Jazanda***-*kivuli/pwani/ufuoni/ndotoni/juu/chini*
iii. ***Msemo***- *umeishi ndani ya kivuli*
iv. ***Tashtiti*** - *Hata huyo Lesulia unajuaje atakuwa mtemi wetu tena? Umeishi ndani ya kivuli cha Lesulia kiasi cha kwamba hujui uchaguzi unabisha?*
v. ***Uhuishi***-*uchaguzi unabisha.*
vi. ***Takriri*** -*Lesulia*
vii. ***Nidaa***-*Umo ndotoni wewe!*
viii. ***Kisengerenyuma/mbinu rejeshi*** - *Wavyele hawakukosea waliposema ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni*
ix. ***Tanakuzi***- *Aliye juu msubiri chini/ ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni*
x. ***Methali***-*ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni/ Aliye juu msubiri chini*
xi. ***Kejeli/dhihaka*** - *Umeishi ndani ya kivuli cha Lesulia kiasi cha kwamba hujui uchaguzi unabisha/ Umo ndotoni wewe!*
xii. ***Taswira*** – *Aliye juu msubiri chini/ ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni*
xiii. ***Kinaya*** - *Aliye juu msubiri chini/ ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni*
xiv. ***Kweli-kinzani*** - *Aliye juu msubiri chini/ ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni*
xv. ***Chuku*** - *Aliye juu msubiri chini/ ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni*
xvi. ***Litifati*** - *Wavyele hawakukosea waliposema ulichokiacha pwani, kakingoje ufuoni.*
xvii. ***Majazi*** – *Lesulia.*

*Zozote 6x1=6*

b) **"Ama kweli, nchi hii huendeshwa na wabinafsi wakubwa!"**

Kwa hoja **kumi na nne**, tathmini ukweli wa kauli hii ukurejelea riwaya *Nguu za Jadi.* (alama 14)

i. ***Watoto kutapika/kuendesha/kudhoofika kiafya*** – *Sagilu anatumia ushawishi wake kuleta maziwa yaliyoharibika nchini kinyume na sharia hivyo waoto wanaendesha na wengine kudhoofika kiafya.*
ii. ***Utekaji nyara*** – *Mtemi Lesulia anatumia vibaya mamlaka yake kumteka nyara Lonare ili ashinde uchaguzi.*
iii. ***Kutengwa kwa wanawake*** – *Mila na tamaduni za Matuo zinahakikisha wanaume wanawatenga wanawake katika nyadhifa za uongozi na hata kuwanyima fursa ya kuhutubu mfano Mangwasha.*
iv. ***Aibu*** – *Mrima anabakia na aibu baada ya Lonare kufichua pesa alizokuwa amepewa na Sagilu kuwasaliti.*
v. ***Kunyanganywa leseni*** – *Mafamba ananyanganywa leseni baada ya kushindwa kesi. Serikali inatumia vibaya mamlaka kufanya hivyo/hakimu pia aliyeamua kesi ya ardhi na kuwarudishia Waketwa ardhi iliyonyakuliwa na Nanzia na Mbwashu anafanyiwa vivyo.*
vi. ***Vifo/mauko*** – *Wafanyibiashara waliompiku Sagilu wanauawa wanapokataa kufuata njama zake za kifisadi.*

vii. ***Ukosefu wa ajira/ubaguzi katika kutoa nafasi za ajira*** *– Mtemi na Wakule wenzake wanatoa ajira kwa mapendeleo hivyo Waketwa wengi wanakosa ajira.*

viii. ***Ukiritimba/mazingira mabovu ya kufanyia biashara*** *– Sagilu anaagiza meli isitie nanga hadi amalize kuuza ngano yake kwa bei ghali.*

ix. ***Kukwepa kulipa ushuru/kunyima taifa pato*** *– Sagilu na wenzake wachache serikalini wanakwepa kulipa ushuru hivyo kunyima taifa pato/Chifu Mshabaha hatimaye anaandamwa kwa kuwa alikosa kulipa ushuru akiwa madarakani.*

x. ***Watu kufutwa kazi*** *– Mangwasha anafutwa kazi kw vile ni Mketwa. Mshabaha anatumia vibaya mamlaka yake kufanya hivyo.*

xi. ***Uharibifu wa mazingira*** *– Matajiri wanachimba migodi na mchanga na kupaacha eneo lile tambarare baada ya kuwahonga viongozi.*

xii. ***Uhuni/Ghasia*** *– Mtemi Lesulia anawahonga vijana ili kuzua rabsha katika uchaguzi asalie madarakani/Sagilu anamtuma Sihaba kwenda kutupa bomu katika arusi ya Mrima na Mangwasha ili kulipiza kiasi ya kukataliwa na Mangwasha.*

xiii. ***Unyakuzi wa ardhi*** *– Nanzia na Mbwashu wanatumia vibaya ushawishi wao kunyakua ardhi ya Waketwa katika eneo la Matango..*

xiv. ***Ukimbizi wa ndani kwa ndani*** *– ardhi ya Waketwa inaponyakuliwa na Nanzia na Mbwashu, wanalazimika kuishi kanisani na katika kambi za wakimbizi.*

xv. ***Ulanguzi/matumizi ya mihadarati*** *– Ngoswe anatumia ushirika wake wa karibu na Mtemi kulangua mihadarati inayowafanya vjana kuacha shule.*

xvi. ***Ufuska*** *– Sihaba anatumia urafiki wake na Sagilu kufungua danguro ambamo ufuska uliendelezwa/Sagilu anahusiana kimapenzi na Cheiya, ambaye ni mkazamwanawe..*

xvii. ***Uhasama/migogoro ya kikabila*** *– Imani za jadi zinazoendelezwa na viongozi kama Mtemi Lesulia za kupeana ajira kwa mapendeleo zinapelekea migogoro kati ya kabila la Waketwa na Wakule.*

xviii. ***Umaskinishaji/unyanyasaji*** *– wananchi wanalazimika kununua bidhaa kwa bei ghali kutoka kwa wakiritimba kama Sagilu hivyo kuzidi kuwa maskini.*

xix. ***Kusambaratika kwa ndoa-*** *Sagilu anamhoga Mrima na pesa zinazomfanya kwenda Ponda Mali na kuweka ndoa yake hatarini.*

xx. ***Ubwete/utepetevu katika malezi/kulewa*** *– Hongo anayopewa Mrima inamfanya kulewa na kutelekeza malezi ya wanawe.*

xxi. ***Jaribio la kuua*** *– Cheiya anapewa vishawishi ili kujaribu kumwuua Lonare.*

xxii. ***Kudorora kwa Uchumi wa taifa*** *– Viongozi kama Sagilu na Mtemi Lesulia wanafisidi mali ya taifa hivyo kunakuwa na nakisi kwenye bajeti kila uchao.*

xxiii. ***Ndege kuanguka*** *– ajira zinazotolewa kwa mapendeleo na Mtemi kwa Wakule pekee inapeekea ndege za jeshi kuanguka.*

xxiv. ***Vyombo kupasuka baharini-*** *ajira zinazotolewa kwa mapendeleo na Mtemi kwa Wakule pekee inapeekea vyombo vya majini vya jeshi kupasuka.*

xxv. ***Kudorora kwa viwango vya elimu-*** *baadhi ya walimu wanaoajiriwa na serikali ya Mtemi Lesulia kwa mapendeleo hawajafuzu hivyo wanaendeleza bora elimu badala ya elimu bora.*

xxvi. ***Kuishi kwa hofu*** *– wananchi wanaishi kwa hofu baada ya Sihaba na kundi lake kulipwa ili kusambaza vijikaratasi.*

xxvii. ***Utamaushi/kutamauka*** *– Waketwa wanaofurushwa makwao wanatamauka kuhusu kupata haki baada ya Nanzia na Mbwashu kunyakua ardhi yao.*

xxviii. ***Kulimbikiziwa viongozi/kuzimwa kwa demokrasia/madikteta kusalia madarakani*** *– Mtemi Lesulia anatumia vibaya mamlaka yake kusalia madarakani kupitia propaganda, uhuni na utekaji nyara.*

xxix. ***Unyakuzi wa rasilimali za taifa*** *– Nanzia anayakua jumba la Skyline Mall la wananchi kwa kutumia ushawishi wake.*

xxx. ***Lawama*** *– Waketwa wanalaumiwa kwa matatizo yanayokumba Wanamatuo kutokana na Wakule kuwa madarakani.*

xxxi. ***Uharibifu wa mali/kuchomewa makaazi*** *– Waketwa wanachomewa nyumba zao ili ardhi yao inyakuliwe na Nanzia na Mbwashu.*

***Za kwanza 14x1=14***

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**Timothy Arege**: *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 4 au 5*

**4.** "… **Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi**. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha." (uk 67)

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

*Msemaji ni* ***Sara*** *kwa* ***Neema*** *wakiwa* ***nyumbani kwao Neema kijijini/nyumbani kwa Yona na Sara.*** *Haya yalitokana na Neema kusema kuwa* ***uvumilivu wa Sara umemsababishia ugonjwa.***

*4x1=4*

b) Jadili umuhimu wa msemaji katika kujenga tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 4)

*Msemaji ni* ***Sara****. Kupitia kwake;*

i. ***Wahusika wengine*** *kama vile Dina, Bela, wafanyikazi wa nyumbani, Yona na Neema wanajengwa.*

ii. *Kupitia kwake,* ***maudhui*** *ya ndoa/uvumilivu/uwajibikaji/nafasi ya mwanamke katika jamii yanajengwa kupitia kwa mateso anayostahimili mikononi mwa Yona.*

iii. *Kupitia kwake,* ***dhamira*** *ya mwandishi ya kuchimuza madhila anayopitia mwanamke/umuhimu wa uvumilivu katika ndoa/mchango wa wanawake katika kustawisha familia unajitokeza.*

iv. *Baadhi ya matukio katika tamthilia yanatokea katika* ***mandhari*** *ya nyumbani kwake na Yona/ametumiwa kujenga* ***mandhari*** *ya hospitalini alikolazwa.*

v. ***Mazungumzo/dayolojia*** *kati yake na baadhi ya wahusika kama vileAsna, Neema, Yona na Dina ni muhimu kwa vile yanatusaidia kuelewa matukio mbalimbali kwenye tamthilia.*

vi. ***(Ploti):*** *Kupitia kwake,* ***migogoro*** *kati yake na Yona inachimuzwa/****mgogoro*** *kati ya wahafidhina wa mila kama yeye na Yona na Wanamapinduzi wanaotaka hali isalie vile/tunakuja kufahamu* ***usuli*** *wa Asna kutakakuwa Tomboy/****usuli*** *wa Yona kulalamikia njaa/tunafahamu* ***mustakabali*** *wa Yona(anapoomba msamaha)/ anajenga* ***mustakabali*** *wa mabinti zake Asna, Neema na Salome waliokuwa wametelekezwa na jamii/****maneno*** *yake yanamhimiza Neema kustahimili machungu katika ndoa/Asna kuacha kumchukia na kumshutumu Bunju.*

*zozote 4x1=4*

**c)** Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha* kwa hoja **kumi na mbili**. (alama 12)

i. ***Afya/siha njema ya Sara*** *haipatikani kwa njia rahisi kwa vile inawagharimu Neema na Bunju kiasi kikubwa cha fedha wanazolipia hospitalini/Bunju na Neema kuzozania kuhusu nani wa kugharamia matibabu ya Sara.*

ii. ***Maisha ya staha/starehe anayoishi Neema*** *yaani nyumba anamoishi na gari analoliendesha zilitokana na bidii za Bunju ikiwemo mikopo kwenye benki anayochukua.*

iii. ***Masomo ya Mina katika shule ya bweni*** *yanatokana na Bunju kujizatiti kumlipia karo. Neema alimshihinikiza kumpeleka katika shule ya bweni.*

iv. ***Ufanisi wa mabinti za Yona masomoni*** *haukuwa rahisi kwa vile Yona na Sara walisimangwa na kutukanwa kwa kujaliwa watoto wa kike na kukosa mrithi. Hatimaye Asna, Salome na Neema wanakuwa nyota ya jaha/kijiji.*

v. ***Ajira ya Yona kama mwalimu*** *ilitokana na miaka yake mingi ya kujizatiti kusoma hasa katika chuo kikuu na kufuzu.*

vi. ***Staftahi ya Bunju na Neema*** *inakuwa tayari kwa wepesi kutokana na kujukumika kwa Bela anayeamka mapema kuandaa kiamshakinywa na kumtayarisha Lei kwenda shuleni.*

vii. ***Kutoweka kwa ugumba/utasa/kupata watoto kwa Yona na Sara*** *kulifanyika baada ya muda mrefu wa kujawa na matumaini na kusali; hata ingawa walikuwa wamesimangwa na kusemwa na wanajamii.*

viii. ***Uinjinia wa mwanawe Beni*** *– Beni anamuenzi mwanawe ambaye ni injinia na kumwonea fahari. Mwanawe ni injinia baada ya kutia bidii kwenye elimu yake.*

ix. ***Uthabiti wa ndoa ya Neema na Bunju*** *unatokea mwishoni mwa Tamthilia baada ya Sara kuwa kwenye mstari wa mbele kuwashauri na hata kumwonya Asna dhidi ya kumchukia Bunju.*

x. ***Kuungama makosa na kuomba msamaha kwa Yona*** *– kunakuja baada ya yeye kuchukua muda kuwazia mchango wake katika ugonjwa wa Sara na kujipata mwingi wa majuto.*

xi. ***Kuacha pombe kwa Yona*** *– kunachukua muda na kutokea baada ya Yona kuwazia mchango wa pombe katika kuathiri na kusambaratisha familia yake.*

xii. ***Kuishi kwa Neema/Kupata shufaa baada ya ajali*** *– Bunju anamwitia Flying Doctors wanaomtibu mpaka hali yake inakuwa shwari, lau angeaga kwa vile ajali yenyewe ilikuwa mbaya sana.*

xiii. ***Ajira thabiti kwa Neema/wanawake kujitegemea*** *– kunajitokeza baada ya Neema kuvumilia masaa mengi ya kazi, misongamano barabarani na hata kuwa na muda mfupi na mwanawe Lemi.*

xiv. ***Kupelekwa out kwa Lemi*** *– kunatokea tu pale ambapo Neema anaweka kando shughuli zake za kikazi ili kutenga muda, inafika mahali anakuwa na shughuli nyingi zinazomlazimu kumtwika Bunju jukumu hilo.*

xv. ***Elimu ya chuo kikuu ya Asna*** *– inamalizika baada ya Asna mwenyewe kuvumilia gharama ya juu ya maisha hasa ada ya nyumba. Halikadhalika, bado anaishi maisha uchwara lakini yenye matumaini licha ya kukosa ajira.*

xvi. ***Ufanisi kwenye ndoa ya Yona na Sara*** *–unajitokeza baada ya Sara kuvumilia mateso, masimango na vipigo vya kila mara, kisa na maana, alishindwa kumzalia Yona mrithi.*

xvii. ***Yona kupata fursa ya kubarizi na wazee*** *– kunatokana na Neema kujinyima na kumtumia hela anazopaswa kutumia kujinunulia dawa, naye anazitumia kujistarehesha na wazee wenzake asionekane shabiki.*

xviii. ***Upishi wa Yona na Sara*** *kijijini umewezeshwa na Bunju na Neema kujinyima kuwanunulia jiko la gesi.*

xix. ***Kuandaliwa kwa chakula cha Yona*** *kunawezeshwa na Dina kuitikia salamu na hata kustahimili moshi unaotoka kwenye kuni zinazotumiwa katika upishi.*

xx. ***Kazi za nyumbani kwa Sara na Yona*** *zinarahisishwa kwa vile Binju na Neema wanajikalifu kuwaajiria wafanyikazi pale nyumbani; ingawa mmoja wa wafanyikazi hao anatoroka eti kazi ziko nyingi na mwingine anaachishwa kazi kwa kukosa uaminifu.*

***Za kwanza 12x1=12***

***(Tanbihi: Aangazie pande mbili, la sivyo, tuza 0)***

**5.** "Sikiliza basi! Zamani mila zetu hazikuruhusu watoto wa kike kuenda skuli au kurithi kitu. Sasa wanakwenda na kurithi. Zamani watoto wa kike walikuwa wanategemea mifuko ya waume zao. Sasa hali ni tofauti. Utamaduni, mila na desturi zetu zinazidi kuyakubali mabadiliko. Thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka. Kuyapuuza haya yote ni kazi bure." (uk 60)

a) Tambua toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

i. ***Kurai/kuhimiza/kuhamasisha/kutumai*** - *Thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka*

ii. ***Kukejei/kudhihaki/kubeza*** - *Zamani watoto wa kike walikuwa wanategemea mifuko ya waume zao/ Zamani mila zetu hazikuruhusu watoto wa kike kuenda skuli au kurithi kitu*

***Kutaja alama 1, ufafanuzi alama 1 (kutaja bila ufafanuzi, tuza 0)***

b) Bainisha umuhimu wa tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

i. ***Msemo*** – *thamani ya mtoto wa kike imepanda; kuonyesha kubadilika kwa hadhi ya mtoto wa kike katika ulimwengu wa sasa ikilinganishwa na awali.*

ii. ***Nahau*** – *kutegemea mifuko; kuashiria utegemezi wa watoto wa kike kwa waume zao katika jumuiya ya awali.*

iii. ***Jazanda*** - *mifuko; kuashiria utegemezi wa watoto wa kike kwa waume zao katika jumuiya ya awali.*

iv. ***Taswira (fiche)*** - *nafasi yake kupanuka/thamani ya mtoto wa kike imepanda; kuonyesha kubadilika kwa hadhi ya mtoto wa kike katika ulimwengu wa sasa ikilinganishwa na awali.*

***(za kwanza 2x2=4; Tamathali na ithibati 1, umuhimu 1)***

c) Fafanua aina **nne** za taswira zinazodhihirika katika dondoo hili. (alama 4)

i. ***Taswira masikizi/sikivu*** - *Sikiliza basi!*

ii. ***Taswira mwendo*** - *kuenda skuli*

iii. ***Taswira oni*** - *thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka.*

iv. ***Taswira hisi*** - *Sikiliza basi!*

*Za kwanza 4x1=4*

d) Thibitisha ukweli wa kauli iliyokolezwa huku ukirejelea tamthilia ya *Bembea ya Maisha.* (alama 10)

i. *Awali, mtoto wa kike* ***hakuruhusiwa kusoma/kupata elimu****. Sara anakosa kwenda shule kwa sababu ya mila na desturi. Sasa, Neema na Asna wanasoma.*
ii. *Awali, mtoto wa kike* ***hakuweza kumiliki wala kurithi mali****. Neema ana nyumba na hata kuendesha gari.*
iii. *Awali, mtoto wa kike* ***aliozwa pindi tu baada ya kubaleghe****. Neema, hatimaye* ***anajichagulia mume*** *atakaye baada ya kusoma na kufuzu.*
iv. *Wanawake* ***waliachiwa tu kazi za jikoni kama vile upishi****. Sasa, wanaajiriwa na kufanya kazi kwa mfano Neema anafanya* ***kazi afisini****.*
v. *Watoto wa kike* ***awali walidharauliwa kwani Sara na Yona wanatukanwa na kusemwa wanapopata watoto wa kike****. Wa kiume walithaminiwa zaidi. Baadaye, Neema na Asna* ***wanathaminiwa*** *na wanakijiji licha ya kuwa wa kike kwa vile wamesoma.*
vi. *Awali,* ***wanaume walikuwa hawawasaidii wake zao katika kazi za nyumba****. Kazi hizo zilionekana tu za wanawake. Yona, hatimaye anamsaidia Sara katika kazi za nyumba Sara anapougua.*
vii. *Awali,* ***wanaume walifanya maamuzi pasi kushauriana na wake zao****. Sasa, Bunju na Neema wanashauriana kabla ya kufanya jambo lolote.*
viii. *Awali,* ***utamaduni ulimkandamiza/inamfinya mwanamke hivi kwamba hangeweza kushindana na mwamaume****. Katika usasa, wanawake waliosoma kama vile Neema na Asna wanaonekana kuwa nyota na mwanga katika kijiji.*
ix. *Neema anajukumika katika* ***kumtibu mamake****, Sara kwa usaidizi wa Bunju. Hali hii inamfanya mwanamke kuonekana kuwa na hadhi/umuhimu ingawa* ***awali wanawake hawakupewa nafasi ya kufanya hivyo.***
x. *Awali,* ***wanawake walitegemea mifuko ya waume wao (kulingana na Beni).*** *Hivi sasa, wanafanya kazi na kujitegemea kwa mfano Neema anafanya kazi katika afisi na kuweza kukimu mahitaji yake.*
xi. *Awali,* ***wanawake walilazimishwa kuingia katika ndoa na kutumikishwa na waume wao kama vile Yona alivyomfanyia Sara****. Sasa, wanawake wana uwezo wa kuishi peke yao bila kuwazia hata suala la ndoa kama vile Asna.*
xii. *Awali,* ***wanawake walisahau familia watokako baada ya kuolewa (Sara anasema Neema si kama wanawake wengine wanaosahau watokako)****. Sasa, Neema anawasomesha nduguze Salome na Asna akisaidiwa na Bunju.*

***Za kwanza 10X1=10***
***(Tanbihi: Aangazie pande mbili, la sivyo, tuza 0)***

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au 7*

**F. M. Kagwa**: *Pupa*

**6.** a) "Dunia ni kama shamba la mihindi, huzaa mahindi na vizimwili. Utakwendaje kuvuna na kukusanya vizimwili badala ya mahindi na kuvipeleka ghalani?" (uk 99)

Kwa kutolea mifano **kumi** kwenye hadithi ya *Pupa* onyesha namna wahusika mbali mbali '*wanavuna na kukusanya vizimwili badala ya mahindi*'. (alama 10)

***i.*** *Mwakuona anawadanganya wazaziwe kuwa anenda shuleni/anaacha shule ili kwenda mjini alikoagizwa na Bi. Mtego.* ***Anaishia danguroni anakotumika vibaya kimapenzi.***

*ii.* *Bi. Mtego anawahadaa wasichana na maghulamu wachanga eti atawatafutia ajira ng'ambo na* ***badala yake anawawazongomeza katika ufuska pale Chenga-ways****.* ***Hatimaye njama zake zinafichuliwa.***

*iii.* *Mwenye Chenga-ways anavuna vizimwili* ***pale ambapo Mwakuona anafanikiwa kutoroka****. Anajizatiti kumtafuta kila mahali kwani Mwakuon alikuwa mhimili mkubwa katika biashara yake.*

*iv.* *Wazaziwe mwakuona wanapata* ***idadi kubwa ya watoto (kumi na wawili) ambao wanashindwa kuwalea*** *jambo linalowafanya wengine kama Mwakuona kuwa kivutio rahisi cha walanguzi kama Bi. Mtego.*

*v.* *Walinzi wa Chenga-ways* ***wanavuna vizimwili pale ambapo Mwakuona anatoroka****. Chuma chao kinakuwa motoni kwa vile wangepoteza kazi zao.*

*vi.* *Serikali inavuna vizimwili* ***inaposawiriwa kufumbia macho biashara chafu kama ile iliyokuwa ikiendelezwa pale Chenga-ways*** *kwa vile imestahiwa na kuheshimiwa.*

*vii.* *Wateja wa wa pale chenga-ways, wanaume kwa wanawake (Maafisa tajika serikalini)waliostawisha biashara ile wanavuna vizimwili* ***kupitia kutoroka kwa Mwakuona kwa vile angeonsha wazi ufuska uliokuwa ukiendelezwa mle*** *hivyo kuwaharibia pa kumalizia ashiki zao.*

*viii.* *Wasichana waliokuwa Chenga-ways walivuna vizimwili badala ya mahindi pale* ***ambapo walihadaiwa na Bi. Mtego na kuacha elimu kwa kisingizio kuwa wangepewa kazi ughaibuni*** *; badala yake, wanaishia danguroni.*

*ix.* *Mashaka ndoto zake zinazimika pale ambapo* ***anatumikishwa Chenga-ways katika ufuska na akaacha shule****. Kwa njia ii, anavuna vizimwili badala ya mahindi.*

*x.* *Walimu wa Mwakuona wanavuna vizimwili badala ya mahindi baada ya* ***Mwakuona kupuuza wosia wao na kufanya maamuzi kwa pupa yanayomwingiza Chenga-ways*** *anakojipata akifanya ukahaba.*

*xi.* *Viongozi wa kidini wa Mwakuona wanavuna vizimwili badala ya mahindi pale ambapo* ***Mwakuona anapuuza waadhia wa kidini na kuuasi utu na kujitwika mapuuza****. Anaishia kujipata kwenye mtego wa Bi. Mtego na kuishia Chenga-ways anakotumikishwa kimapenzi.*

*xii.* *Wazaziwe Mwakuona wanavuna vizimwili badala ya mahindi pale ambapo* ***wanakwenda kumsaka na hawana picha yake yoyote. Aidha, walikuwa hawana pesa za kuwanunulia polisi mafuta kwenye gari ili wamsake*** *hivyo juhudi zao zinaambulia patupu.*

xiii. *Mwakuona, anapokuwa chumbani na mwanaume aliyelipa kujihusisha naye kimapenzi, anavuna vizimwili badala ya mahindi pale ambapo* ***juhudi zake za kukataa kitendo hicho zinapoambulia patupu.***

***Zozote 10x1=10***
***(Tanbihi: Aangazie pande mbili, la sivyo, tuza 0)***

**Phibbian Muthama**: *Nilitamani*

b) ***Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata : (uk 87)***

*Nataka niwe na yule, aishiye pa kherini,*
*Na kasri kama lile, lin'towe majonzini,*
*Na kazi kama ile, nijikimu maishani,*
*Nataka na gari lile, nitaabishe mjini.*

i. Tambua maudhui **kuu** inayotawala kifungu ulichopewa. (alama 1)

***Maudhui ya tama -*** *Nataka na gari lile, nitaabishe mjini.*

***1x1=1 (bila ithibati, tuza 0)***

ii. Bainisha madhara ya maudhui uliyoitambua katika swali la 6b (i) ukirejelea hadithi *Nilitamani*. (alama 9)

*i.* ***Ulaghai/uongo/ulaghai*** *– Tumaini anamdanganya utingo wa daladalakuwa pochi lake liliibwa na kwamba alikosa nauli hivyo akabebwa bila kulipia.*
*ii.* ***Utegemezi/kulimbikizia wengine mahitaji*** *– Tumaini anawatwika Jenifa na Nina majukumu ya kumlisha na kukimu mahitaji yake.*
*iii.* ***Kuhamahama*** *– Tumaini anaishi kwa Nina kwam muda na kisha kuhamia kwa Jenifa baada ya kukosa ajira madhubuti hivyo alikuwa akihamahama.*
*iv.* ***Uharijuzi/uhamiaji*** *– Tumaini anahama kutoka nchini Kenya kwenda Tanzania kutafuta ajira. Tamaa ya kupata riziki inamsongomezea Tanzania.*
*v.* ***Kutelekeza malezi*** *– Tumaini anamwachia bibi yake jukumu la kumlea mwanawe Radhi ili afike Tanzania kutafuta ajira.*
*vi.* ***Kutamauka*** *– baada ya kukosa kazi, Tumaini anabaki akiwa mwingi wa mafadhaiko, amepoteza matumaini na anawazia kurejea kwao nyumbani.*
*vii.* ***Majuto*** *– Tumaini anajawa na majuto kuhusu kilichomtoa Kenya kumpeleka ugenini kutafuta ajira kwa sababu milango ya heri ilikataa kunfungukia.*
*viii.* ***Mapuuza -*** *Tumaini anamwachia bibi yake jukumu la kumlea mwanawe Radhi ili afike Tanzania kutafuta ajira.*
*ix.* ***Kuhatarisha maisha*** *– Tumaini anajipata pabaya peponi ambako alikuwa atolewe kafara kwa vile alimezwa na tamaa ya kumpenda Romeo, kijana aliyekuwa amekutana naye siku hiyo.*
*x.* ***Wepesi wa kushawishika/pupa/kughalifika/kuhadaika -*** *Tumaini anashawishika kwa wepesi kujiingiza katika mahusiano na Romeo, kijana ambaye ndiyo alikuwa amekutana naye kwa mara ya kwanza siku hiyo.*
*xi.* ***Msongo wa mawazo-*** *Tumaini anajipata akijiuliza maswali mengi baada ya kushindwa kupata ajira. Anawazia hata pendekezo la kurudi kwao.*
*xii.* ***Kujipagaza ufuska/kutamani waume wa wengine*** *– Tumaini anamtamani mumewe Nina.*
*xiii.* ***Kutotosheka/kutoridhika/kutamani zaidi*** *– Tamaa ya Tumaini inamtia kutamani zaidi na anapanda ngazi kutoka kutamani hadi kutaka.*

xiv. ***Aibu/soni-*** *Tumaini, baada ya kukosa pesa za kununulia chakula, anaaibika kurejea kwa Jenifa.*

xv. ***Kupoteza muda*** *– Tumaini anapoteza muda mwingi akibarizi na kutumai kuwa hali yake ingeimarika; fikra ambazo zinachochewa na tamaa ya maisha bora.*

xvi. ***Vibarua duni*** *– Tumaini yuko radhi kufanya hata vibarua duni kusudi atimize mahitaji yake yanayochochewa na tamaa.*

xvii. ***Kusalitiwa/kugeukwa*** *– Romeo anamgeuka Tumaini wanapofika mandhari ya peponi na kutaka kumtoa kafara.*

xviii. ***Uzembe*** *– tama inamfanya Tumaini kukosa kujukumika kutafuta kazi na badala yake kukesha akitumai kuwa angepata vya bwerere.*

***zozote 9x1=9***

**Yussuf Shoka Hamad**: *Mzimu wa Kipwerere*

**7.** a) Jadili jinsi mwandishi alivyotumia taharuki kufanikisha vipengele vifuatavyo katika hadithi *Mzimu wa Kipwerere*:

*Taharuki ni mbinu ya kusimulia au kuandika riwaya au hadithi kwa kufanya hadhira na/au wahusika wajawe na hamu ya kutaka kujua likochotokea baadaye; hamu ya kutaka kuendelea kusoma /kusikiliza. Kwenye hadithi Mzmu wa Kipwerere, taharuki imetumika kufanikisha mandhari na wahusika ifuatavyo:*

**i. Mandhari (alama 6)**

***i. Kuchipuka kwa Mzimu kutokana na kaburi la Kipwerere kunamtia msomaji hamasa ya kutaka kujua zaidi Mzimu ulivyojiotea.***

1. ***Mandhari ya Mzimuni*** *yanajengwa kwani tunapata kujua usuli wake.*
2. *Vilevile,* ***mandhari ya makaburini*** *yanajengwa kwani kaburi la Kipwerere lilijitokeza katikati ya makaburi mengi ambako wanajamii mashuhuri walizikwa.*
3. *Aidha,* ***mandhari ya kuzimu*** *yanachimuzwa kwa vile wanajamii wanaamini kuwa kwa vile Kipwerere alikuwa na nguvu za kishetani, anakuwa na mamlaka na hata kuishi baada ya kufa kupitia kaburi lake kujiotea na kuwa Mzimu.*

***ii. Wanaovunja mwiko na kukiuka kanuni za Mzimu kutolewa kafara kunazua taharuki.***

1. ***Mandhari ya Mzimuni*** *yanajengwa; uzito ukiwa sababu za kuchiwa kwake zinachimuzwa.*

***iii. Majibu ya wazee kuhusu sauti za watu kule Mzimuni na harufu ya sigara na tumbaku kutoka mle yanazua taharuki akilini mwa Msimulizi.***

1. ***Mandhari ya akilini mwa Msimulizi*** *yanachimuzwa kwani anakuwa na mshawasha wa kufahamu ukweli kuhusu yanayojiri Mzimuni.*
2. *Vilevile,* ***mandhari ya Mzimuni*** *yanachimuzwa kwani matukio yatokeayo mle yanapigwa msasa mawazoni mwa Msimulizi.*

iv. ***Mwananume na mwanamke wanaoimba na kuingia Mzimuni siku moja kabla ya Msimulizi kumfumania Salihina na kisha wanapoondoka kila mmoja anashika njia yake hivyo kuchochea ilhamu ya Msimulizi kutaka kujua zaidi kuhusiana na Mzimu.***

1. ***Mandhari ya Mzimuni*** *yanajengwa. Wimbo unaoimbwa kabla ya kuingia mle unazidisha hofu na sabau za kuchiwa kwa Mzimu.*

v. ***Bishoo anazimia anapofumaniwa na Msimulizi. Inawatia wasomaji kuwa na ari ya kutaka kujua zaidi yaliyomtendekea.***

1. ***Mandhari ya Mzimuni*** *yanachimuzwa. Bishoo anazimia kado ya kitanda cha besera baada ya kufumaniwa na Msimulizi. Matukio mle yanadhihirika.*

vi. ***Salihina anaponaswa na tawi la mti kisha akaanza kuomba radhi kunamtia msomaji ilhamu ya kutaka kufahamu kilichompata asubuhi iliyofuata.***

1. ***Mandhari ya mtini*** *Salhina anakoning'inia yanajengwa. Salihina anafikiri kuwa Msimulizi ndiye aliyemshikilia hivyo anamwomba msamaha.*
2. ***Mandhari ya Mzimuni*** *pia yanachimuzwa kwa vile mti alioning'inia Salihina upo pale Mzimuni.*

***Zozote 6x1=6***

**ii. Wahusika** **(alama 6)**

i. ***Kuchipuka kwa Mzimu kutokana na kaburi la Kipwerere kunajenga wahusika ifuatavyo:***

***Wanakijiji*** *wanasawiriwa kuwa:*

i. ***Wahafidhina/watamaduni*** *– wanaamini pasi kuuliza maswali kuwa kaburi la Kipwerere liliota na kuwa Mzimu.*
ii. ***Washirikina*** *– wanaamini pasi kuuliza maswali kuwa kaburi la Kipwerere liliota na kuwa Mzimu.*
iii. ***Wajinga*** *– hawawajibiki kuchunguza ukweli kuhusiana na kaburi la Kipwerere mchango wake katika kuota kwa Mzimu.*
iv. ***Wenye mapuuza/wepesi wa kushawishika*** - *hawawajibiki kuchunguza ukweli kuhusiana na kaburi la Kipwerere mchango wake katika kuota kwa Mzimu.*
v. ***Wenye hofu/waoga*** *– wanaogopa kaburi la Kipwerere kwa kuwa ndicho chanzo cha Mzimu wa Kipwerere.*

ii. ***Wanaovunja mwiko na kukiuka kanuni za Mzimu kutolewa kafara kunazua taharuki.***

*Hivyo,* ***wanakijiji*** *wanasawiriwa kuwa:*

i. ***Waoga*** *– wanaamini kuwa wangevunja miiko wangetolewa kafara.*
ii. ***Wenye mapuuza*** *– hawachunguzi zaidi iwapo waliovunja miiko awali walikuwa chakula cha mashetani kama ilivyodaiwa.*
iii. ***Wajinga*** - *hawachunguzi zaidi iwapo waliovunja miiko awali walikuwa chakula cha mashetani kama ilivyodaiwa.*
iv. ***Wahafidhina/watamaduni***- *wanaamini kuwa wangevunja miiko wangetolewa kafara kwa mizimu.*
v. ***Washirikina*** - *wanaamini kuwa wangevunja miiko wangetolewa kafara kwa mizimu.*

**iii. *Majibu ya wazee kuhusu sauti za watu kule Mzimuni na harufu ya sigara na tumbaku kutoka mle yanazua taharuki akilini mwa Msimulizi.***

*Msimulizi anasawiriwa kuwa:*

i. ***Mpekuzi*** *– anakataa katakata kuamini wanayoyasema wazee kuhusu mashetani kuvuta sigara na kutumia tumbaku.*

ii. ***Mdadisi wa mambo*** *– majibu anayopewa na wazee yanachochea ilhamu ya kujua mengi zaidi kuhusu yanayoendelezwa Mzimuni.*

iii. ***Jasiri*** *– majibu ya wazee yanamchochea kwenda karibu na Mzimu ili ajifunze wimbo ambao ni ufunguo wa kuingia mle.*

iv. ***Mwanamapinduzi*** *– anakataa kuamini majibu ya wazee kuwa mashetani wana familia na hutumia vileo na tumbaku. Badala yake, anahisi kuwa kuna mapya anayopaswa kuchunguza mle hadi hatimaye anawafumania Salihina na Bishoo.*

***Watoto wenzake*** *wanasawiriwa kuwa:*

i. ***Waoga*** *– wanaamini wanachoambiwa na wazee kuwa Mzimuni mna mashetani.*

ii. ***Wajinga*** **-** *wanaamini wanachoambiwa na wazee kuwa Mzimuni mna mashetani.*

iii. ***Wepesi wa kushawishika*** **-** *wanaamini wanachoambiwa na wazee kuwa Mzimuni mna mashetani.*

iv. ***Watiifu*** **-** *wanaamini wanachoambiwa na wazee kuwa Mzimuni mna mashetani.*

***Wazee wanasawiriwa kuwa:***

i. ***Waongo/Laghai*** *– wanawahadaa watoto wanaouliza kuhusu sauti zitokeazo Mzimuni kuwa ni shetani na mkewe wanaojiandaa kuhusu maisha yao ya usoni na ya watoto wao.*

ii. ***Wanafiki-*** *wanawahadaa watoto ingawa wanajua kuwa wanachosema ni uongo.*

iii. ***Wasiri-*** *siri ya yanayoendelea Mzimuni kama ulanguzi na matumizi ya mihadarati wanaificha.*

***Wanajamii wanasawiriwa kuwa:***

i. ***Wenye mapuuza*** **-** *hawawajibiki kutafitia ulanguzi na matumizi ya mihadarati yanayoendelezwa Mzimuni licha ya kusikia harufu kutoka mle.*

ii. ***Wajinga*** **-** *hawawajibiki kutafitia ulanguzi na matumizi ya mihadarati yanayoendelezwa Mzimuni licha ya kusikia harufu kutoka mle.*

**iv. *Mwananume na mwanamke wanaoimba na kuingia Mzimuni siku moja kabla ya Msimulizi kumfumania Salihina na kasha wanapoondoka kila mmoja anashika njia yake hivyo kuchochea ilhamu ya Msimulizi kutaka kujua zaidi kuhusiana na Mzimu.***

***Wanasawiriwa kuwa:***

i. ***Walevi/wapenda anasa*** **-** *punde tu baada ya kuingia mle, harufu ya tumbaku inasikika.*

ii. ***Wanafiki*** *– wanatumia mihadarati Mzimuni licha ya kufahamu kuwa ni pahali patakatifu panapofaa kuchiwa.*

iii. ***Wajanja*** **-** *wanatumia mihadarati Mzimuni licha ya kufahamu kuwa ni pahali patakatifu panapofaa kuchiwa.*

iv. ***Wenye vitisho*** *– wimbo wanaoimba kabla ya kuingia Mzimuni unatisha kwani wanasema jinsi wanavyowala watu hai.*

***v. Bishoo anazimia anapofumaniwa na Msimulizi. Inawatia wasomaji kuwa na ari ya kutaka kujua zaidi yaliyomtendekea. Anasawiriwa kuwa:***

i. ***Mwoga*** *– anapofumaniwa, anazimia zii mpaka asubuhi.*

***vi. Salihina anaponaswa na tawi la mti kisha akaanza kuomba radhi kunamtia msomaji ilhamu ya kutaka kufahamu kilichompata asubuhi iliyofuata.***
***Salihina*** *anasawiriwa kuwa:*

i. ***Mwenye majuto*** *– anaomba msamaha na kusema kuwa ni mara yake ya kwanza kwenda Mzimuni.*

i. ***Mwoga*** *– anapiga mayowe akiomba asemehewe na asitiriwe.*

ii. ***Mwenye soni/aibu*** *– anaomba kuzikwa duniani na kufunikwa ahera/anaomba kusitiriwa ili asipate aibu inayoambatana na kufumaniwa.*

iii. ***Mwongo*** *– anadanganya kuwa ilikuwa mara yake ya kwanza kwenda mle Mzimuni.*

iv. ***Mnafiki*** *– anadanganya kuwa ilikuwa mara yake ya kwanza kwenda Mzimuni na kuwa hakuwa peke yake.*

***Zozote 6x1=6***

***(Tanbihi : Ataje na kufafanua mfano wa taharuki kisha abaini mchango wake katika kujenga wahusika na mandhari. Bila, tuza 0)***

**Mzamane Nhlapo**: *Nipe Nafasi*

b) Eleza tafsiri **nane** za kichwa cha hadithi '*Nipe Nafasi'*. (alama 8)

i. *Wanawake kama Mama Kazili wanaomba* ***nafasi ya kujifanyia maamuzi*** *kama vile kubadilisha mazingira, kuwatembelea jamaa zao na kukaa huko kwa muda watakao.*

ii. *Wanawake wanaomba* ***nafasi ya kujieleza kinagaubaga bila kukandamizwa****. Mama Kazili anaomba nafasi ya kuskizwa hata baada ya maamuzi kufanywa kwenye Kraal.*

iii. *Wanawake* ***wanaomba nafasi ya kusoma/kupata elimu*** *– Mama Kazili anaomba nafasi ya kujiendeleza kimasomo; anasoma na kuwa mwalimu wa chekechea na kuweza kukimu mahitaji ya wanawe.*

iv. *Wanawake wanaomba* ***nafasi ya kuishi maisha ya staha/kuwapa wanao maisha mazuri*** *– Mama Kazili anajiwekea ahadi kuwa wanaume wanaposhindwa kukimu mahitaji ya familia, angefanya kila awezalo kuhakikisha kuwa ameboresha maisha yake na ya wanawe.*

v. *Wanawake wanaomba* ***nafasi ya kujitafutia riziki/kupata/kutafuta ajira*** *– Mama Kazili anaomba nafasi ya kuachwa ajitafutie kazi wanawe wanapokuwa kwa Matweba; na mwishoni mwa mwaka huo anakuwa mwalimu wa chekechea na kuweza kukimu mahitaji ya wanawe.*

vi. *Wanawake wanaomba* ***nafasi ya kujiinua kiuchumi*** *– kwa mujibu wa Mama Kazili, wanawake wananyimwa fursa ya kujiinua kiuchumi na kuchukua mikopo.*

vii. *Wanawake wanaomba* ***nafasi ya kulalama/kulalamika/kuweka wazi malalamishi yao*** *– Mama Kazili analalamika kuwa Moshe hawajibiki kuwatunza wanawe ingawa anapuuzwa na wazaziwe Moshe/Kuna mwanamke Habelo aliyeuawa na mumewe kwa vile alikuwa amelalamika waziwazi kuwa mumewe alikuwa mzembe.*

viii. *Wanawake wanaomba nafasi ya kupewa **nafasi ya kujitetea wanaposhutumiwa/ kabla ya kuhukumiwa** – Mama Kazili anajitetea waziwazi licha ya uamuzi wa Kraal kuwa wa mwisho na usioweza kubatilishwa.(uk 80)*

ix. *Wanawake wanaomba **nafasi ya kulindwa na katiba** – Mama Kazili anasimama kidete na kusema kuwa ingawa ni raia wa Swaziland, ana haki ya kuwa raia wa Lesotho kupitia kwa ndoa yake na Moshe. (uk 80)*

x. *Wanawake wanaomba **nafasi ya kukosoa matumizi ya dini kuwakandamiza** – Mama Kazili anakubali kuwa Bibilia inasema wake wanapaswa kuwaheshimu waume zao ila anasisitiza kuwa waume nao wana majukumu wanayopaswa pia kutenda. (uk 80)*

xi. *Wanawake wanaomba **nafasi ya kujitetea dhidi ya mila kandamizi** – Mama Kazili anawahamasisha wajinasue kutoka kwenye mikatale ya mila na tamaduni zinazomchukua mwanamke kama mtoto na anyepaswa kuwa chini ya himaya ya mwanaume. (uk 80)*

xii. *Wanawake wanaomba **nafasi ya kujiamulia kisiasa**- Mama Kazili anasema kuwa Chama cha Taifa cha Basutoland kimekuwa kikiendeleza hila dhidi ya wanawake huku kikidai kuwa kilichaguliwa na wanawake; kwa misingi hiyo, jamii na serikali zilikuwa zinawanyima uhuru. (uk 80)*

xiii. *Wanawake wanaomba **nafasi ya kutafuta ufadhili au mikopo** ili kujiinua – Mama kazili anadai kuwa wanawake wananyimwa nafasi ya kutafuta ufadhili au mikopo. (uk 80)*

xiv. *Wanawake wanaomba **nafasi ya kutembelea marafiki**. Mama Kazili anadai kuwa wanawake wananyimwa fursa ya kutembelea jamaa na marafiki. (uk 80)*

*Za kwanza 8x1=8*

## SEHEMU E: USHAIRI

**8.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata*:**

Barabara bado ni ndefu
Nami tayari nimechoka tiki
Natamani kuketi
Ninyooshe misuli
Nitulize akili

Lakini

Azma yanisukuma
Mbele ikinihimza kuendelea
Baada ya miinuko na kurubo
Sasa naona unyoofu wake
Unyoofu ambao unatisha zaidi

Punde natumbukia katika shimo
Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena
Ghafla nakumbuka ilivyosema
Ile sauti zamani kidogo
"Kuwa tayari kupanda na kushuka"

Ingawa nimechoka
Jambo moja li Dhahiri
Lazima nifuate barabara
Ingawa machweo yaingia
Nizame na kuibuka
Nipande na kushuka
Jambo moja nakumbuka: Mungu
Je, nimwombe tena? Hadi lini?
Labda amechoshwa na ombaomba zangu
Nashangaa tena!

Kitu kimoja nakiamini
Lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua mpya
Nijiokote kuiandama hii barabara yenye ukungu
Nikinaswa na kujinasua
Yumkini nitafika mwisho wake
Ikiwa wangu mwisho haitauwahi kabla.

**Timothy Arege**: *Tunu ya Insha*

***Maswali***

a) Taja mambo **saba** yanayokatisha tamaa katika shairi hili (alama 7)

*i. Barabara ndefu*
*ii. Kuchoka sana*
*iii. Panda-shuka za maisha.*
*iv. Kutumbukia katika shimo*
*v. Sauti za zamani yenye kumbukumbu.*
*vi. Ukosefu wa siha.*
*vii. Kuingia kwa machweo.*
*viii. Maombi kutojibiwa na Mungu.*
*ix. Kifo/mauko.*

*za kwanza 7x1=7*

b) Tambua toni katika shairi. (alama 2)

*i.* ***Toni ya kutamauka*** *– ikiwa wangu mwisho haitawahi kabla.*
*ii.* ***Toni ya matumaini/kutumai/kurai/himizo/kuhamasisha*** *– kuwa tayari kupanda na kushuka/azma yanisukuma, mbele ikinihimiza kuendelea.*

*Kutaja alama 1, ufafanuzi alama 1 (kutaja bila ufafanuzi, tuza 0)*

c) Kwa kutoa mifano, tambua aina **mbili** za urudiaji kisha uonyeshe umuhimu wake. (alama 4)

*i.* ***Urudiaji wa sauti/silabi:****.* ... ***ku****ibuka*
...***ku****shuka*

*Kuleta wizani/mahadhi/ridhimu/uimbikaji wa shairi/sauti /n/ kusisitiza nafsi rejelewa*

*ii.* ***Urudiaji wa kimuundo:*** *...natamani kuketi*
*...ninyooshe misuli*
*...nitulize akili*

*Kusisitiza maudhui ya kutamauka*

iii. ***<u>Urudiaji wa neno</u>*** *– barabara ; kuonyesha maisha magumu anayopitia.*

iv. ***<u>Urudiaji wa kimaana:</u>*** *...natamani kuketi*
*...ninyooshe misuli*
*...nitulize akili*
*Kusisitiza maudhui ya kutamauka*

*(aina na ithibati 1, umuhimu 1)*

d) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 3)

i. *Shairi hili lina beti sita.*
ii. *Shairi hili lina kipande kimoja.*
iii. *Idadi ya mishororo betini inatofautiana/inabadilikabadilika katika kila ubeti.*
iv. *Vina vinabadilikabadilika kutoka mshororo mmoja hadi mwingine.*
v. *Mshororo wa mwisho unabadilikabadilika katika kila ubeti/lina kiishio/halina kibwagizo.*
vi. *Lina mistari mishata.*

*zozote 3x1=3*

e) Andika ubeti wa **mwisho** kwa lugha nathari. (alama 4)

*Mshairi* ***<u>anaamini</u>*** *kuwa lazima* ***<u>ajitahidi</u>*** ***<u>kuandama maisha haya ya changamoto</u>*** *na* ***<u>kujinasua ili kufaulu kabla ya mauti</u>*** *kumkumba.*

*4x1=4*